

KUCHOP NI POWER!

JE, UNAPATA WAPI HABARI KUHUSU NGONO?

Elimu hii haihusu ngono tu! Inapaswa kukusaidia wewe kama kijana kujifunza kuhusu:



Watafiti walichunguza jinsi Kenya inavyotoa mafunzo ya kina kuhusu elimu ya ngono katika kaunti za Nairobi, Mombasa na Homa Bay katika mwaka wa 2015. Waliwahoji zaidi ya wanafunzi 1000 wa kidato cha pili na tatu, walimu na walimu wakuu kutoka shule 78.

Ukweli ni kwamba wakati wa uchunguzi wetu, robo ya wanafunzi - ambao wengi wao wana umri wa miaka 15 hadi 17 - walikuwa tayari wamefanya ngono. Wanafunzi wanataka - na wanahitaji - habari kuhusu jinsi ya kuzuia mimba zisizotakikana, virusi vya ukimwi na magonjwa mengine ya zinaa.

Ni nini inafunzwa shuleni? Hii hapa ni orodha ya yale ambayo watafiti waligundua:

- Habari isiyo kamili na ambayo wakati mwingine si kweli ndiyo inayofundishwa. Wengi wa walimu waliohojiwa walisema kuwa wanasisitiza katika masomo yao kuwa kutofanya ngono ndiyo njia bora zaidi au pekee ya kuzuia mimba na magonjwa ya zinaa. Hata hivyo, utafiti unaonyesha kuwa programu zinazokataza ngono pekee hazifaulu
- Ni asilimia 20 pekee ya wanafunzi waliojifunza kuhusu njia mbalimbali za kuzuia kupata mimba kama kondomu au tembe za kupanga uzazi, na hata wachache zaidi ndio walikuwa wamejifunza jinsi ya kuzitumia na zinakopatikana
- Walimu wengi (asilimia 59) walisema pia kuwa walisisitiza sana kuwa kufanya ngono ni hatari na ukosefu wa maadili kwa vijana
- Wanafunzi wawili kati ya watatu (asilimia 67) wanataka muda zaidi utengewe kwa ajili ya elimu ya ngono. Pia, wanaonelea kuwa ingekuwa bora zaidi wanalifunzwa mapema zaidi wakiwa katika shule za msingi

MADA 4 KUU AMBAZO WANAFUNZI WANGEPENDA KUJIFUNZA ZAIDI KUZIHUSU NI KAMA:



Walimu wanapenda kutumia mihadhara na maongezi. Lakini, wanafunzi hawapendi mbinu hii kwa sababu inachosha. Wanapenda mbinu bunifu zaidi za kufundisha na zinazowahusisha kama:



Mitandao ya kijamii au matumizi ya intaneti



Video



Michezo ya kuigiza na drama



Miradi ya sanaa




Densi



Mashairi na masimulizi

Karibu wanafunzi wote waliichukulia elimu ya ngono kuwa muhimu au muhimu sana katika maisha yao ya kibinafsi. Asilimia 30 ya wanafunzi walisema kuwa hawakupokea habari hii kutoka kwa wazazi wao. Kwa hivyo, vijana hupata wapi habari hii nje ya shule?



Kinachohitajika ni nini?

- Shule zinafaa kuzingatia vilivyo elimu ya ngono! Ni muhimu kwa wanafunzi kupewa habari za kweli kabla ya kuanza kufanya ngono ili waweze kufanya maamuzi ya busara
- Kuyafanya mafunzo ya ngono kuwa ya kusisimua kwa kutumia njia bunifu na zinazowashirikisha vijana
- Walimu wanafaa kuwa tayari kujibu maswali kuhusu elimu ya ngono na uzazi kutoka kwa wanafunzi - au kuwaelekeza kwa mtu mwingine aliye tayari kuyajibu. Vijana wangependa kupewa ushauri kuhusu jinsi ya kuwa na mahusiano bora na jinsi ya kushughulikia msukumo kutoka kwa wenzao

Una maswali? Ugependa kujifunza zaidi?

Unaweza kuwasiliana nasi katika Facebook kwenye Kukachora au One2OneKe

Unaweza pia kutembelea vituo rafiki kwa vijana vya Family Health Options Kenya vinavyopatikana huko Eastleigh, Nairobi na Bombolulu, Mombasa.



African Population and Health Research Center